



Mwaliko wa
KONGAMANO LA KISWAHILI LA THELATHINI NA TATU
Bayreuth tarehe 22 Mei hadi 24 Mei 2020

Wenzetu wapendwa, wapendwa washiriki, ndugu na marafiki,

Ni furaha yetu kuwaalikeni nyote kwa Kongamano la Kiswahili la thelathini na tatu!

Tangu hapo mwaka wa 1987, ambapo kongamano la kwanza lilifanyika ili kusherehekeea miaka 100 ya ufundishaji wa Kiswahili vyuoni hapa nchini Ujerumani, Kongamano la Kiswahili limepiga hatua nyingi. Kongamano letu ni madhirikano ya kipekee ya kila mwaka yanayofanyika Iwalewahaus, Chuo Kikuu cha Bayreuth. Mkutano huu unatoa fursa kwa yejote yule aliye mtaalamu wa masomo mbalimbali yanayohusu utafiti na uchunguzi wa vipengele kadha wa kadha vya lugha ya Kiswahili, fasihi na tamaduni za Afrika Mashariki barani Afrika na ughaubuni. Hivyo basi, tunawakaribisheni tena wote ambao huja hapa Bayreuth katika miaka iliyopita na pia tutafurahi sana kuwapokea na kuwakaribisha wataalamu, wanafunzi na mashabiki wapya katika kongamano lijalo.

Mada kuu ya kongamano la 2019

Kongamano hili linalenga kumulika mada kuu ifuatayo: Masomo ya Kiswahili Duniani.

Nia kuu ya Kongamano la Kiswahili la thelathini na tatu ni kuwaalika wataalamu wa Kiswahili kutoka vituo mbalimbali vya masomo ya Kiswahili duniani (hususan kutoka nchi za kusini) ili tujadiliane kuhusu nyanja na fani za Masomo ya Kiswahili. Tujiulize masomo ya Kiswahili ni nini haswa.

Kiswahili hakishindi lugha nyingi za kiafrika kwa idadi ya wazungumzaji wake kwenye bara la Afrika na vilevile ng'ambo tu. Tena Kiswahili ni lugha ambayo inafundishwa katika vyuo vikuu vingi zaidi kuliko lugha nyingine za Kiafrika. Pia kumekuwa na utaaluma mwingi kuhusu lugha yenyewe, pamoja na fasihi, historia na utamaduni wake. Zaidi ya Afrika Mashariki na Ulaya na Marekani, China, Japani, Brazil na vilevile Korea, Mexico, Urusi, Iran, Ghana, Zimbabwe na Afrika Kusini zimefundisha lugha ya Kiswahili pamoja na fasihi na

utamaduni. Vipo vituo vya radio, wachapishaji wa vitabu na siku hizi haswa vyombo ya habari vya kijamii katika nchi za magharabi, lakini vilevile, zimekua kwenye nchi kama, kwa mfano, China na Iran, ambazo zimezidi kutia mkazo kwenye Masomo ya Kiswahili.

Kongamano letu la Kiswahili la Bayreuth ni kioo cha maendeleo hayo: Limezidi kuwavuta wataalamu na walimu wa Kiswahili kutoka kila pembe ya dunia na kutoka fani na masomo mbalimbali. Kongamano lilipoanzishwa miaka thelathini na tatu zilizopita liliwalenga wataalamu na walimu wa Kiswahili kutoka vyuo vikuu vya Ujerumani. Lakini hatua kwa hatua kongamano lenyewe limewakaribisha watu kutoka nchi nyingi na vilevile limepanua kwa upana wa fani: Zaidi ya wanaisimu na wanafasihi, wanaanthropolojia, wanaakiolojia, wanajiografia, wanahistoria na wanafalsafa walanza kuja. Kulinganishwa na mwanzo wake wakati mfumo wa lugha na matini zake zilikuwa ni mada ya kipekee, vipengele na mitazamo zinazozungumzwa zimekuwa nyingi zaidi.

Mwaka wa 2020, tunataka kujadiliana kuhusu vipengele hivi viwili: uwingi wa masomo ya Kiswahili duniani na mabadiliko kwenye mitazamo na mijadala zake. Swali la msingi ni: Masomo ya Kiswahili ni nini haswa? Bila ya shaka, hatumainishi ufundishaji wa lugha peke yake, lakini vilevile maendeleo ya utafiti wa aini nyingi unaohusu lugha, fasihi na tamaduni kwa maana pana zaidi. Tumeona maendeleo gani ya kihistoria? Hali yake ya siku hizi ni ipi na yataendelea vipi katika miaka ijayo? Tukilinganisha vyuo mbalimbali kuna tofauti gani duniani na zipi zinalingana na zipi zinabishana? Vipi Masomo ya Kiswahili yanarejelea nyanja nyingine za kitaalamu za kijirani zinazokaribiana na mijadala yao: Kwa mfano, kuna uhusiano gani baina ya Masomo ya Kiswahili na Masomo ya Kiafrika kwa jumla? Masomo ya Kiswahili inachukua nafasi gani kwenye mijadala mikubwa kuhusu “Area Studies” (“utafiti wa maeneo”) ya siku hizi? Tukiangalia utawala wa Kiingereza kwenye utaalamu kwa julma siku hizi na ukosefu wa mtazamo wa kilugha kwenye masomo ya baadaya-ukoloni (“postcolonialism”), kwa upande mmoja, na shauku ya kutia mkazo kwenye uwingi wa ujuzi kutoka maeneo ya kusini, yaani epistemolojia za kusini (“southern epistemologies”), kwa upande mwingine, Kiswahili kitapata kuchangia vipi kwenye miaka ijayo?

Tukiwaza masomo ya Kiswahili kwa ndani, pia inatubidi kuijuliza kuhusu mapengo, makosa na upofu za utaalamu wetu pamoja na nyayo za ukoloni na baadaya-ukoloni (postcolonialism). Kwa mfano, Afrika Mashariki na Ulaya, masomo na ufundishaji wa lugha zilianzishwa na wakoloni. Kwa hivyo, tunawezaje kuzingatia historia na urithi huu siku hizi? Pia tuisahau mazingira ya siku hizi ambapo Kiswahili kimepata mashiko kinachotenga lugha nyingine. Vipi mitazamo ya kila mtaalamu inayoathiriwa na mengi inachangia kwenye namna yake ya kuendeleza masomo ya Kiswahili?

Mada nydingine

Tumependekeza mada hii kuu hapo juu iwe ndiyo mada kuu ya kujengea mijadala yetu kwenye kongamano la 2020, lakini kama mjuavyo, Kongamano la Kiswahili Bayreuth halibani washiriki katika sehemu zilizotajwa tu. Kwa hiyo, pia tunawaombeni msisite kupendekeza michango mingine ya vipengee vinavyorejelea lugha, fasihi au tamaduni za maeneo ya Kiswahili; kwani Kongamano la Bayreuth linalenga nyanja tofauti tofauti na vile vile ni fursa iliyo wazi kwa michango yoyote ile inayohusu Kiswahili, Uswahili na Waswahili kwa jumla.

Usajili

Tafadhali tumeni makala katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Kila wasilisho litapewa muda wa dakika thelathini tu; ambamo dakika ishirini ni za kuwasilisha na dakika kumi ni za majadiliano na hadhira. Tafadhali jiandikishe kwa baruapepe kupitia *swahili@uni-bayreuth.de* na ututumie kichwa (angaa cha awali) cha makala mpaka **tarehe 15 mwezi wa Februari mwaka wa 2020**. Iwapo utawasilisha kwa Kiswahili, tutumie pia muhtasari wa makala kwa Kiingereza. Tunawaomba wote kujiandikisha hata ikiwa mtashiriki bila ya kuwasilisha makala.

Pahala na Wakati

Pahala pa Kongamano hili ni Iwalewahaus, kituo cha masomo ya Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Bayreuth, iliyoko kwenye Wölfelstraße 2, kuanzia tarehe 22 Mai hadi 24 Mai 2020.

Wasilianeni nasi bila kusita iwapo mna maswali yoyote. Kwa mambo yote yanayohusu kongamano tafadhali tumieni anwani yake ya barua pepe; yaani *swahili@uni-bayreuth.de*

Karibuni nyote! Salamu nydingi,

Ni watayarishi wenu

Serena Talento, Nikitta Adjirakor, Dyoniz Kindata, Duncan Tarrant, Okwiri Oduor and Clarissa Vierke

Swahili Colloquium

Prof. Dr. Clarissa Vierke

Literaturen in afrikanischen Sprachen

Universität Bayreuth

95440 Bayreuth

Telefon: + 49 921 55-3550

Fax: + 49 921 55-3641

Email: swahili@uni-bayreuth.de